FASIHI SIMULIZI

UTABIRI WA KCSE

Maswali ya Marudio Matarajiwa Katika Mtihani Mkuu wa KCSE.

MARUDIO KATIKA SEHEMU YA FASIHI SIMULIZI.

SERIES 1

Ukihitaji majibu,
Pigia Bw. Isaboke 0746 222 000
AU *0742 999 000*

MWALIMU CONSULTANCY

UTABIRI WA KCSE 0746 222 000

USHAIRI SIMULIZI.

1) Fafanua kwa tafsili Nyimbo za kidini.

2) Jadili sifa za Nyimbo za kidini.

3) Fafanua Umuhimu wa nyimbo za kidini.

4) Fafanua sita tano za Tumbuizo

5) Jadili Umuhimu wa nyimbo za tumbuizo.

6) Eleza maana ya Hodiya / chapuzo.

7) Jadili sifa sita za hodiya katika jamii

8) Fafanua umuhimu wa hodiya.

9) Eleza maana ya Nyimbo za mapenzi.

10) Taja sifa zozote nane za myimbo za mapenzi

11) Fafanua umuhimu wa nyimbo za mapenzi.

12) Jadili Umuhimu wa nyimbo za vita.

13) Fafanua maana ya Kongozi.

14) Fafanua sifa na umihimu wa kongozi katika jamii

15) Eleza maana ya Bembea/ bembelezi / pembejezi.

16) Zitaje sifa nane za Bembelezi

17) Jadili Umuhimu wa bembea.

18) Nyimbo za kisiasa huwa na umuhimu na sifa kadhaa. Zitaje

19) Taja Sifa za nyimbo za watoto.

20) Fafanua majukumu ya nyimbo za watoto

21) Fafanua maana ya nyimbo zifuatazo

- **a.** nyimbo jaadiya.
- **b.** kimai.
- **c.** wawe/ vave
- **d.** Tenzi..

22) Eleza umuhimu wa nyimbo katika jamii.

0746 222 000

MASIMULIZI / HADITHI

1) Jadili umuhimu wa ngano za mazimwi.

2) Eleza maana ya Ngano za mtanziko.

3) Jadili Umuhimu wa ngano za mtanziko.

4) Fafanua maana Ngano za usuli.

5) Mighani ni nini?

6) Fafanua sifa bainifu za Mighani

7) Jadili Umuhimu wa mighani katika jamii

8) Eleza maana ya Mbazi.

9) Fafanua maana ya Istiara.

10) Eleza sababu nne za Kufifia kwa hadithi.

MAIGIZO

1) Eleza umuhimu wa miviga katika jamii.

2) Eleza udhaifu wa miviga katika jamii ya sasa

3) Nini maana ya ngomezi katika fasihi simulizi.

4) Eleza sifa zozote tano za ngomezi.

5) Eleza vizingiti vya ngomezi.

6) Huku kitoa mifano, eleza dhima zozote tano za ngomezi.

7) Fafanua Udhaifu wa ngomezi.

8) Eleza maana ya Michezo ya watoto.

9) Fafanua Sifa za michezo ya watoto.

10) Eleza Umuhimu wa michezo ya watoto.

11) Fafanua maana ya Matambiko.

12) Taja sifa kadhaa za matambiko

0746 222 000

SEMI.

2) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya misimu/simo katika fasihi simulizi.

3) Fafanua sifa zozote tano za misimo.

4) Eleza uamilifu /majukumu mbalimbali ya misimu katika jamii.

5) Huku ukitoa mifano eleza mbinu zozote tano zinzotumiwa kuunda misimu.

6) Fafanua mchango au nafasi ya misimu katika sarufi ya kiswahili

7) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya lakabu katika fasihi simulizi.

8) Fafanua vigezo mbalimbali vinavyosababisha kuundwa kwa lakabu.

9) Eleza sifa za lakabu katika jamii.

10) Eleza umuhimu wa lakabu katika jamii.

MASWALI YA FASIHI SIMULIZI

1. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

1. Angole angole mwanangu

Mwanangu nakuchombeza

Nakuchombeza ulale

Ulale ukiamka

Nikupikie ubwabwa

Na mchuzi wa papa

Ukilia waniliza, wanikumbusha

Ukiwa wa baba na mama

2. Baba na mama watende

Ilimu kunikatizia

Ng'ombe, mbuzi kupokea

Kunioza dumu kongwe

Haliuki na halende

Kazi kupiga matonge

3. Likingia mvunguni

Lavunjavunja vikombe

Likilala kitandani

Languruma kama gombe

0746 222 000

a) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. **(alama 2)**

b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. **(alama 5)**

c) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu**.** **(alama 3)**

d) dBainisha shughuli mojamoja ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. **(alama 2)**

e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa manne ya kutumia mahojiano. **(alama 4)**

f) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia nne ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. **(alama 4)**

2. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

"Mwanangu, dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu…"

a) Tambua na ueleze kipera hiki cha fasihi **(alama 2)**

b) Eleza sifa tatu za kipera hiki. **(alama 3)**

c) Fafanua dhima tano za kipera hiki katika jamii. **(alama5)**

d) Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake? **(alama 4)**

e) Eleza utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. **(alama 6)**

3. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata***

Katiechi Analia, Katiechi Analia
Chozi lausaliti undani wake
Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka
Undani ambao japo anachelea kutangaza asije akaonekana apendaye
chongo… Itabidi kuutoa, kuumwaga mtama

Na kiini cha chozi hili ni kwamba imewadia
Imewadia siku ya siku kanisani kwenda,

0746 222 000

Kujitia pingu

Kujitia pingu, pingu za aushi

Je, hakuyataka haya?

Hakupania yapakata kama mwanagenzi,

Apatakavyo malaika mikononi pake?

Kwani basi analovya, kidari kwa maji

chumvi? Shavu lake laini,kuwa kijivu kwa

shaka?

Ama ni yano mapenzi yalomlemea?

Mapenzi alopalia kwa miaka na dahari?

Kipi kinokwinamisha,

Kwa tewengu kukubwaga?

Ama ni majukumu kuhofia mwenzetu?

Ni adha za ulezi?

Ni hofu ya kutelekezwa?

Jikoni kuachwa jukumu la kawaida?

Ama ni ugeni kwa nasaba uso asili unokuuguza?

Je, ni mazoea unochelea kuacha?

Ama ni uzito wa nanga ua huba?

Kipi, sema ewe mwenzangu,

sema.

Nikahi ni sitara

Usumbufu kuepuka vipanga na mwewe

Ndoa huneemesha na jina kukupa utatukukuka

kimwana Shujaa ukapata wa kukulinda

Miliki ni hakikisho kutoka kwa dume hata katika

mauko, Penzi halali kupata, na warithi kuambulia,

Wa kiume kukufaa

0746 222 000

Silie mwana silie,
Watutia simanzi
Waitia ndoa doa, nuksani kukuandamia.

Wavyele mpeni Baraka
Mashangazi mtemeeni mate
Viganjani kumiminia pumzi zenu za neema
Ndoa yake kutengenea
Maumbu acheni
Kulengwa na machozi
Mwamliza zaidi, unyonge kumtia
Baba mtu mshike kondooyo,
Mwongoze kidesturi, madhabahu karibia,
Mkabidhi mkweo, mwenzi wake wa maisha.

Ndiye takayekuwa fahali, simba atakuwa
kikaida Amri tatoa yeye, malkia kufuata,
Utashi wake tatimizwa, ndivyo sheria inenavyo
Bila yeye kutamka mtamba aandamwi na sahibu
Tampenda ewe kinda, tanyenyekea bila
kulalama

Penzi talinda wewe, wengine sije paramia
Kukupoka mwamba wako!

MASWALI

a) Ainisha utungo huu kimaudhui. **Alama 1**

b) Eleza sifa **tatu** za utungo huu. **Alama 3**

c) Chambua mitindo katika utungo huu. **Alama 4**

d) Unanuia kuwasilisha utungo huu jukwani, tathmini vipengele **sita** ambavyo utavizingatia ili kufanikisha mawsilisho yako. **Alama 6**

0746 222 000

e) Eleza manufaa **manne** ya ndoa kutokana na wimbo huu. **Alama 4**

f) Jamii ina matarajio yepi kuhusu wanandoa? **Alama 4**

4. Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kweye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia 'My friend, kunywa soda.'

a) Bainisha kipera cha utungo huu **(alama1)**

b) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika katika kifungu hiki **(alama3)**

c) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita **(alama6)**

d) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Teteta kauli hii. **(alama5)**

e) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? **(alama5)**

5. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

Hapo zamani za kale Nyani alikuwa rafiki wa kufa kuzikana na Bafe. "Mjukuu wangu sijui kama umewahi kuwazia urafiki wa aina hii; ule wa mmoja wao akijikwaa dole anayeuhisi uchungu wenyewe ni mwenzake."

Wanyama hawa waliishi pamoja kwa amani na upendo. Walisaidiana wakati wa dhiki na wakati wa furaha. Walisaidiana na wakati wa masika na wakati wa kiangazi. La Nyani lilikuwa la Bafe na la Bafe lilikuwa la Nyani. Ulifika wakati ambapo wanyama wote walikumbwa na ngambi ya chakula kutokana na kiangazi kilichoselelea nchini mwao kwa takribani miezi minane.

"Njaa hii itatusafirisha jongomeo," akasema Nyani akiwa ameshika tama.

"Usiwe na wasiwasi ndugu!" akasema Bafe, "Nina hakika kwamba Mwenyezi Mungu hatatuacha tuangamie pamoja na aila zetu."

Kutokana na uchechefu huu wa chakula, Nyani na Bafe pamoja na vikembe wao walikula hadi chakula kile walichokuwa wameweka akiba na kukimaliza. Sasa kuiona kesho ilibaki mikononi mwa Mungu alivyokuwa ametakadamu kusema Bafe kwa maana

0746 222 000

wanyama walianza kupukutika mmoja baada ya mwingine kama majani makavu msimu wa kiangazi. Msitu wote ulijaa nyamafu.

Nyani alipoona kuwa huenda akakata kamba aliamua kula mayai ya sahibuye Bafe wakati alipokuwa ameenda kuhemera ili angalau apate chakula cha kupunguza mng'ato wa njaa. Bafe aliporudi, Nyani alimpiga mafamba kwamba kuchakuro aliyavamia mayai yake na kuyala lakini Bafe hakuridishwa na jibu hili. Aliona hila katika jibu la Nyani na kutaka kubaini ukweli kwani ukweli unapodhihiri uongo hujitenga.

Nyani alipomwona Bafe akimkaribia ili kukinusa kinywa chake, alianza kutoroka bila kukimbizwa na yeyote. Kutoroka kwake kulimthibitishia Bafe kuwa Nyani ndiye aliyekula mayai yake, hivyo akaamua kumfuata unyounyo akiwa amepandwa na kiruu mithili ya Mbogo aliyejeruhiwa usasini. Nyani alikimbia na kujibanza kwenye jiti aina ya bobo liliokuwa karibu na jito lililojaa Ngwena na Viboko.

Bafe aliutumia uwezo wake wa kunusa na kugundua alikojificha Nyani. Nyani alipomwona Bafe akiukwea mti, alishikwa na mtapo na kuanza kutetemeka kama dondoo aliyevamiwa na siafu. Alitamani kuchupa na kupiga kachombe kwenye yale maji male ili atorokee ng'ambo ya pili lakini akagundua kwamba Mamba walikuwa wamekenua meno yao wakimsubiri. Alipotaka kuchupia mti wa msonobari uliokuwa karibu naye, pia chui watatu walikuwa wamelalama kwenye matawi ya mti huo wakimsubiri mithili ya golikipa anayeusubiri mpira ili audake. Alipotamani kushuka, aligundua kwamba naye Bafe alikuwa akiupanda mti kwa kasi akiwa amefunua kinywa tayari kummeza. Je, ungekuwa Nyani, ungefanya nini?

MASWALI

(a) Huku ukitolea ithibati, ainisha ngano hii:

i. Kimaudhui **(alama 2)**

ii. Uhusika **(alama 2)**

(b) Tambua na ufafanue umuhimu wa mbinu za utambaji zilizotumika kufanikisha uwasilishaji wa ngano hii. **(alama 6)**

(c) Eleza manufaa ya kutumia mbinu ya mahojiano kukusanya data ya fasihi simulizi. **(alama 5)**

(d) Fafanua njia **tano** ambazo kwazo jamii ya kisasa inaendeleza utanzu wa hadithi. **(alama 5)**

0746 222 000

6. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

" Kwa taadhima na ruhusa yenu, wapenzi, ninasema hivi: kwamba thawabu ya mja ni sawasawa na jitihada na suna zake. Siku nyingi tumewinda. Na silalamiki kwa kuwa adinasi kwa kawaida huwinda mengi katika sayari hii kwa kadri ya haja na hekima yake. Hana budi, hata hivyo kutumia ubongo wake kwa namna ambavyo Jaliya alivyomkirimu. Naam! Kwa maana wenye hekima hunaswa kwenye hila zao. Nawaomba kwa hivyo mmakinike, pasiwe kwenu faraka bali mhitimu katika nia moja na ushauri mmoja katika ombi letu. Asenteni!"

MASWALI

(a) Tambua kipera hiki. Fafanua jibu lako. **(alama 2)**

(b) Fafanua muundo wa kipera ulichosoma. **(alama 3)**

(c) Eleza njia zozote mbili ambazo mtafiti wa kipera hiki anaweza kutumia kukusanya data kukihusu. **(alama 4)**

(d) Taja changamoto moja kwa kila mbinu za ukusanyaji data ulizotaja katika swali la (c) **(alama 2)**

(e) Eleza nafasi ya fanani katika fasihi simulizi. **(alama 4)**

(f) Eleza sifa nne za mwasilishaji bora wa fasihi simulizi. **(alama 5)**

7. Mwanangu twaa
waadhi Pamoja na yangu
radhi Mungu
atakuhifadhi Akuepue na
balaa

Twaa nikupe hirizi

Uifungeto kwa
uzi Uipe na
taazizi Upate
kuyangalia
Yangu
utakaposhika
Mwanangu
hutosumbuka Duniani
utavuta

0746 222 000

Na alihira utakia
Na ulimi wa thawabu
Uwe mtu mahababu
Kule utakapoingia

La kwanda kamata
dini Faradhi usukhini
Na suna ikimhini
Ni wajibu kuitia

Pili uwe na adabu
La tatu uwe wa
kusadiki Uambiwalo
ulitii
Mtu asoshika haki
Siandamene naye
njiani.

MASWALI

a) Kwa kutumia kigezo cha dhamira, ainisha kipera hiki. **(Al.2)**

b) Jadili sifa za jamii ya utungo huu. **(Al.4)**

c) Fafanua toni ya nafsi neni katika utungo huu. **(Al.2)**

d) Jadili sifa za kimuundo zinazozingatiwa wakati wa uwasilishaji wa kipera hiki. **(Al.3)**

e) Eleza mambo manne ambayo nafsi nenewa anafaa kuzingatia ili kufanikisha uwasilishaji wakipera hiki. **(Al.4)**

f) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hoja tano utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. **(Al.5)**

8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Malaika
Nakupenda malaika x2
Ningekuoa malaika...
Ningekuoa dada...
Nashindwa na mali sina wee...
Ningekuoa malaika x2
Pesa, zasumbua roho yangu x2
Nami niafanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee...
Ningekuoa malaika x2

0746 222 000

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui**. (alama 2)**

(b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. **(alama 2)**

(c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. **(alama 6)**

(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.

i. Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii**. (alama 5)**

ii. Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

9. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Mfalme ana watoto wawili wa kiume na anataka mmoja wao amrithi. Kwa sababu hataki kupendelea yeyote, anawapa changamoto ya kukimbia hadi mji wa mbali kwa farasi wao. Yule ambaye farasi wake atafika mwisho ndiye atakayemrithi. Ndugu hawa wanazembea jangwani kwa siku kadha kwa sababu kila mmoja anataka kufika wa mwisho. Hatimaye wanakutana na mzee mwenye busara ambaye anawapa wosia. Wanapanda farasi upesi na kutoka mbio ili wafike kwenye mji wa mbali walioagizwa na baba yao. Je, Mzee mwenye busara aliwaambia nini?

MASWALI

a) i) Tambua kijipera **(alama 1)**

ii) Taja sifa za kijipera hiki **(alama 4)**

iii) Wewe ni mmoja wanaowasilishiwa kipera hiki. Taja mambo Matano utakayoyafanya ufanikishe uwasilishaji huu. **(alama 5)**

b) Soma utungo ufuatao kisha hujibu maswali yanayofuata

Mtoto ni kito mzigo mzito

i) Tambua kijitanzu **(alama 1)**

ii) Eleza manufaa ya kukirithisha kijitanzu hiki kwa vizazi vijavyo **(alama 4)**

iii) Kipera hiki kinaendelea kudidimia katika jamii yako eleza mbinu tano utakazotumia kukidmisha katika jamii yako. **(alama 5)**

0746 222 000

10. ***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali***

Hapo zamani za kale Nyani alikuwa rafiki wa kufa kuzikana na Bafe.Mjukuu wangu sijui kama umewahi kuwazia urafiki wa aina hii ;ule wa mmoja wao akijikwaa dole anayeuhisi uchungu wenyewe ni mwenzake.

Wanyama hawa waliishi pamoja kwa amani na upendo.Walisaidiana wakati wa dhiki na wakati wa furaha.Walisaidia na wakati wa masika wa kiangazi .La Nyani lilikuwa la Bafe na la Bafe lilikuwa la Nyani.Ulifika wakati ambapo wanyama wote walikumbwa na ngambi ya chakula kutokana na kiangazi kilichoselea nchini mwao kwa takriban miezi minane.

“Njaa hii itatusafirisha jongomeo,”akasema Nyani akiwa ameshika tama.

“Usiwe na wasiwasi ndugu!”akasema Bafe,”Nina hakika kwamba Mwenyezi Mungu hatatuacha tuangamie pamoja na aila zetu.”

Kutokana na uchechefu huu wa chakula ,Nyani na Bafe pamoja na vikembe wao walikuwa hadi chakula kile walichokuwa wameweka akiba na kukimaliza.Sasa kuiona kesho ilibaki mikononi mwa Mungu alivyokuwa ametakadamu kusema Bafe kwa maana wanyama walianza kupukutika mmoja baada ya mwingine kama majani makavu msimu wa kiangazi

.Msitu wote ulijaa nyamafu.

Nyani alipoona kuwa huenda akakata kamba aliamua kula mayai ya saibuye Bafe wakati hadi chakula cha kupunguza mng’ato wa njaa.Bafe aliporudi ,Nyani alimpiga mafamba kwamba kuchakuro aliyavamia mayai yake na kuyala lakini Bafe hakurudishwa na jibu hili.Aliona hila katika jibu la Nyani na kutaka kubaini ukweli kwani ukweli unapodhihiri uongo hujitenga.Nyani alipomwona Bafe akimkaribia ili kukinusa kinywa chake ,alianza kutoroka bila kukimbizwa na yeyote.Kutoroka kwake kulimdhibitishia Bafe kuwa Nyani ndiye aliyekula mayai yake,hivyo akaamua kumfuata unyounyo akiwa amepandwa na kiruu mithili ya Mbogo aliyejeruhiwa usasini.Nyani alikimbia na kujibanza kwenye jiti aina ya bobo liliokuwa karibu na jito

0746 222 000

lililojaa Ngwena na Viboko.

Bafe aliutumia uwezo wake wa kunusa na kugundua alikojificha Nyani.Nyani alipomwona Bafe aliukwea mti,alishikwa na mtapo na kuanza kutetemeka kama dondoo aliyevamiwa na siafu.Alitamani kuchupa na kupiga kachombe kwenye yale maji male ili atoroke ng'ambo ya pili lakini akagundua kwamba Mamba walikuwa wamekenua meno yao wakimsubiri.Alipotaka kuchupia mti wa msonobari uliokuwa karibu naye,pia kwamba Chui watatu walikuwa wamelalama kwenye matawi ya mti huo wakimsubiri mithili ya golikipa anayesubiri mpira ilii audake.Alipotamani kushuka,aligundua kwamba naye Bafe alikuwa akiupanda mti kwa kasi akiwa amefunua kinywa tayari kummeza.Je,ungekuwa Nyani,ungefanya nini?

MASWALI

a) Hii ni ngano ya mtanziko.Thibitisha. **(alama 2)**

b) Fafanua mbinu sita ambazo mtambaji ametumia kuufanikisha uwasilishaji wa ngano hii. **(alama 6)**

c) Eleza aina tatu za taswira zinazojitokeza katika ngano hii. **(alama 3)**

d) Eleza majukumu manne ya fomyula ya ufunguzi katika utungo huu. **(alama 4)**

e) Wewe ni kati ya wanaotambiwa ngano ya aina hii.Fafanua mambo matano ambayo wewe na wenzako mnaweza kuchangia wakati wa utambaji. **(alama 5)**

11. Mababu zetu waliturithisha heshima, utu, utamaduni wa amani, imani na upendo. Tunatambua nia yao njema ya kuona jamii ikiishi kwa utulivu, umoja, mshikamano na uelewano. Leo hii nyuso zetu zimesawijika. Nyuso zimeinama kwa matokeo mabaya ya kitendo cha ubinafsi, unyama na ukatili cha mmoja wetu. Kama jamii, kama watu wa ukoo

wa Shani wa Miramba, tunajitenga na ila hii. Tunamkana Kaliko wa Ndaya. Damu yake si yetu. Tunakemea na kulaani kitendo chake cha ubakaji. Tunalaani umaluuni huu kwa kinywa kipana. Mababu zetu wamemkataa. Mungu wetu mwenye kutaka heri kwa waja wote atuepushe adhabu na ghadhabu yake. Tunaomba dua kwako Mungu wa Mlima mkuu uliovikwa kofia ya theluji na kutukuka. Yalinde mashamba yetu tupate

0746 222 000

mazao mazuri; ila iliyoingia kwetu isije na kiangazi. Mawindo ya usasi wetu yasitupotelee kutokana na kasoro hii. Tunaomba mito yetu isikauke tusikose kitoweo humo na maji kwa mifugo wetu. Bariki ukoo wetu mtukuka. Tubaki imara kama mwamba. Ukoo wetu ni nyota siku zote. Ndiyo ni nyota! Ukoo wa Shani wa Miramba udumu milele!

MASWALI

a) Bainisha kipera cha utungo huu na utoe ushahidi wako. **(alama 2)**

b) Taja sifa zozote tano za kipera hiki. **(alama 5)**

c) Kipera hiki kina nafasi gani kwa jamii? **(alama 5)**

d) Mwasilishaji wa kipera hiki anahitajika kuwa wasifu upi ili kukifanikisha? Fafanua kwa hoja tano. **(alama 5)**

e) Jamii inayohusishwa kifunguni inajiendelezaji kiuchumi? **(alama 3)**

12. ***Soma wimbo huu ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuatia kisha ujibu maswali yanayofuatia.***

1. asiyetaka nimwoe kageni wa
micheni Anaweza kuteremsha jua
alikalie
Lau siyo, amchukue chatu,
Amtumie kusuguliameno

2. sijawaahi kumwona mwingine kama
yeye Nikimwandama haniambii chochote
Kisa na sababu ni nyinyi mahsidi
walionichongea Mwacheni kama hanipendi
aniambie yeye

3. kama inabidi ntumie hirizi
Nitaitumia ili kageni
anipende Pendo lake
halinitoki moyoni
linanisakama na laniuaua

0746 222 000

4.namwomba daktari ,aliye na dawa
anipe Anipe dawa si ya mauti bali ya
mapenzi Tafadhali daktari nitengenezee
Nahisi ni mashakani sababu ya lake penzi

MASWALI

a) Huku ukithibitisha jibu lako,eleza huu ni wimbo wa aina gani **alama4**

b) Tumia mifano maalumu kueleza sifa za utungo wa aina hii **alama8**

c) Fafanua mbinu mbiliza lugha zilizotumika katika wimbo huu **alama4**

d) Taja na ueleze amali kuhusu jamii zinazojitokeza katika wimbo huu ***alama4***

13. Mimi ni Shikwekwe mwana wa
Amuli Ninaitwa simba mwana wa
Matioli Ningurumapo waoga hukimbilia
mbali. Ukali wangu washindana na
pilipili Nishikapo adui zangu
Hata wakibeba sime na mkuki
Hujinyia na kuomba samahani
Nimevikomoa vichaka vya msumbiji
Nimekomesha na Angola
majangili Mwana wa Amuli
nawika!

a)

i) Ainisha kipera cha utungo huu **.(alama 2)**

ii) Jadili sifa zinazopambanua tungo za aina hii za Fasihi simulizi. **(alama 3)**

iii) Bainisha mbinu za kimtindo zinazojitokeza kwenye dondoo hili**.(alama 3)**

b) " wagombanao ndio wapatanao"

i) Andika kipera cha utungo ulioandikwa hapo juu. **(alama 1)**

ii) Tambua fani iliyotumika katika utungo huu **(alama 2)**

iii) Eleza muundo wa kipera hiki **(alama 2)**

c) Kipera hiki kina sifa ya utegemezi na huingiliaana na tanzu nyingine. Thibitisha.

(alama4)

0746 222 000

d) Una nia ya kufanya utafiti kuhusu kipera hiki katka jamii fafanua mbinu utakazotumia kuhifadhi kipera hiki kwa matumizi ya vizazi vijavyo.**(alama3)**

14. ***(a) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Kila kukicha mashaka
Ni kero hili si huba
Mimi pendo la viraka, heri demu la
mkoba Ingawa mno nataka, kuishi nawe
muhiba Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Kamwe sitoshughulika
Nawaje wenye kuziba
Viumbe wanosifika,kwa fedha, chuma na shaba
Walostaarabika, si mimi wa tobatoba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Naapa sitojitweka
Limenichosha si haba
Nasomba vyangu viraka, nitie kwenye
mkoba Sikuye ya kuzinduka, mjinga hawi
juba Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

i) Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha. **(alama 1)**

ii) Eleza sifa **mbili** za nafsi nenewa katika wimbo huu. **(alama 2)**

iii) Fafanua mbinu **tatu** ambazo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wake.**(alama3)**

iv) Eleza faida **nne** za kurithisha wimbo huu kwa vizazi vijavyo. **(alama 2)**

(b) Unanuia kufanya utafiti kuhusu utungo wa maigizo :-

0746 222 000

i) Eleza hatua **tatu** utakazofuata katika utafiti wa utungo huu. **(alama 3)**

ii) Unanuia kutumia **hojaji** kutafitia utungo huu. Eleza **umuhimu** na **udhaifu** wa kutumia njia hii. **(alama 2)**

(c) Bainisha toni ya utungo huu. **(alama 1)**

(d) Fafanua mbinu **nne** ambazo nafsineni itatumia kufanikisha uwasilishaji wake.**(alama 4)**

(e) Eleza mambo ambayo yatapotea wimbo huu ukiandikwa. **(alama 3)**

(f) Ingawa nyimbo zina faida kwa wanajamii, zina madhara pia.Yaeleze madhara manne. **(alama 2)**

15. "Vijana wetu, nyinyi ni taa zetu na nawaomba mnisikilize kwa makini. Sisi kama wazazi wenu tumeona mengi katika ulimwengu huu. Madhumuni ya kuwaita hapa ni kuwashauri msijiunge kwenye mambo ya dunia pasi kutathmini madhara ya myafanyayo kisha mkaishia kulia kilio cha mbwa mdomo juju! Watiini wazazi wenu na msikize sana mashauri yako kwani mkikosa kuyasikia mtapigwa na fimbo ya dunia mje mjute baadaye. Daima iacheni dini iwe taa yenu, ibaki miguuni mwenu milele ndipo iwaangazie njia, mtofautishe jema na baya na linalofaa na lisilofaa. Sisi kama wazazi wenu tunawaomba mbadilishe mienendo ili muishi maisha mema. Nawatakia Baraka za Mola katika safari yenu ya maisha"

MASWALI

a) Ainisha kitanzu hiki cha fasihi simulizi **(ala 2)**

b) Eleza sifa tano zinazotambulisha kitanzu hiki cha fasihi simulizi **(ala 5)**

c) Eleza muundo unaotumika katika uwasilishaji wa kitanzu hiki cha fasihi simulizi**(ala 3)**

d) Fafanua majukumu yanayotekelezwa na kitanzu hiki katika jamii za kileo **(ala 10)**

16. Ma mkwe:

Lena, umekosea
Kutoroka nyumbani,
bila ruhusa
ya wazazi.
Si vyema.

0746 222 000

Lena:

Sijakosea,

Tulisikilizana ila

Maagano, ma mkwe, wanayavunja wao,

Kulazimishwa sitaki, tena nikahi na jizee mithili ya

babu! Mie ngefanyaje?

Ma mkwe:

Ngeenda kwa mashangazi,

Wakuzungumzie kwa wazee,

Banati, rudi kwenu,

Ili uje vizuri,

Hapa kwangu hutakaa,

Lawama sitaki!

Lena:

Ma mkwe, sirudi,

Kwani penzi limenoga,

Kwani Nkosi ananipenda,

na mahari anayo,

wasinisinye

Kwa jizee Karaha, siendi ng'o!

Ma mkwe:

Ole wako Lena,

adhabu yaja kama dhoruba,

Itakuangukia

Mwanangu rudi!

Lena:

Sawa ma mkwe, kesho mafungulia

ng'ombe, taondoka,

Ila, nakusihi, twende nawe!

0746 222 000

MASWALI

a) Tambua kipera kikuu kinachojitokeza katika utungo huu kwa kutolea sababu**. (alama 1)**

b) Utungo huu unaweza kuwekwa katika tanzu mbili za fasihi simulizi. Zitambue.**(alama 2)**

c) Eleza sifa tatu za kipera ulichokitambua. **(alama 3)**

d) Bainisha toni ya kifungu hiki. **(alama 2)**

e) Fafanua mgogoro katika utungo huu. **(alama 2)**

f) Fafanua sifa mbili za mrejelewa katika utungo huu. **(alama 2)**

g) Bainisha tamathali mbili za usemi katika kifungu hiki. **(alama 2)**

h) Fafanua majukumu yoyote matatu ya watu wazima kwa kurejelea kifungu hiki.**(alama 6)**

17. ***Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali***

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na
mito Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti

Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba
moja Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika

0746 222 000

Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka

Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama

wakakimbia Mkuki wangu ulipaa kama umeme

Wote wakalala

Mifugo wakanifuata…

Mko wapi vijana

Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

MASWALI

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako **(al. 2)**

b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu **(al. 2)**

c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni **(al. 4)**

d) Fafanua sifa nne za kipera hiki **(al. 4)**

e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. **(al. 4)**

f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia **(al. 4)**

18. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Malaika

Nakupenda malaika x2

Ningekuoa malaika...

Ningekuoa dada...

Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

Pesa, zasumbua roho yangu x2

Nami niafanyeje, kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

0746 222 000

MASWALI

a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. **(alama 2)**

b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. **(alama 2)**

c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. **(alama 6)**

d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.

i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

19. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Zimepita siku ayami
Siku chungu tangu giza lipotanda
Wakati lipotazama kwa kiwewe na shauku
Pumzisho kipania, roho kupigania
Ziraili alipokakamaa aushiyo kufakamia.

Nilikwita kwa sauti
Ela mpenzi hukunitika
Machoyo litunga mbele
Kumkabili huyu nduli
Nikabaki kunyongonya
Jaala kitumainia,
Mtima kijiinamia
Hatima kungojea.

Ya mwisho lipopumua,
Alfajiri ya kiza kuu
Nalidhani wanichezea,
Mizaha yako kawaida
Lijaribu kupulizia
Hewa toka langu pafu,

0746 222 000

Tumaini kiniambia pumzi zangu takuhuisha
Sikujua hizo likuwa juhudi za mfa maji muhebi.

Macho libaki kutunduiya, tabasamuyo
kitaraji Kumbe mwenzangu kaniacha!
Ukiwa ulinivaa, ukungu ukatwandama
Pa kuegemea sikujua fundo chungu
linisakama Tabibu alipoingia na kutangaza
rasmi mauko.

Ilikuwa kana kwamba ndo jana lipofunga nikahi,
Kumbukizi zilinijia kwa chozi teletele
Japo kifo ni faradhi ndwele hino halieleweki
Ama jicho la hasidi,
Limekuangaza jamani?
Koja hili ninalokuwekea,
Kando ya kasri hili la shakawa
Ni hakikisho toka kwangu, nitatamba sana
njia Kutafuta alotwendea kinyume kutupoka,
Mauko kutuleteya.

a) (i) Ainisha utungo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. **(alama 1)**

(ii) Andika sababu **tatu** kuthibitisha jibu lako la a(i). **(alama 3)**

b) Bainisha sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa katika utungo huu. **(alama 2)**

c) Fafanua vipengele **vinne** vya kimtindo ambavyo vimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. **(alama 4)**

d) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hoja **tano** utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. **(alama 5)**

e) Unanuia kutumia mbinu ya kushiriki kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza sababu **tano** za kuchagua mbinu hii. **(alama 5)**

0746 222 000

20. ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.***

Dunia hii ina matatizo x2

Watu wengi hawajajua

Ni dunia yataabu

Hata hivyo usijali.

Karibu malaika karibu x2

Mimi nikukaribishe

Kwa mikono yote miwili

Dunia mti mkavu.

Usilie mtoto usilie x2

Kwa kuiona dunia

Iliyo na masumbuko

Umebebwa miezi tisa.

a) Huu ni wimbo wa aina gani? **(alama 1)**

b) Eleza ujumbe wa wimbo huu. **(alama 2)**

c) Eleza sifa za nyimbo za bembea . **(alama 4)**

d) Taja tanzu kuu nne za fasihi simulizi. **(alama 4)**

e) Unanuia kukusanya data za kipera kilicho hapo juu. Pendekeza njia tano utakazotumia. **(alama 5)**

f) Eleza changamoto nne utakazokumbana nazo katika kukusanya data zako**. (alama 4)**

0746 222 000

Ukihitaji majibu,

Pigia bw. Isaboke

0746 222 000

MWISHO

0746 222 000

SET BOOKS AVAILABLE WITH US

- ✓ *Artist Of The Floating World*
- ✓ *Bembea Ya Maisha*
- ✓ *Mapambazuko Ya Machweo*
- ✓ *Nguu Za Jadi*
- ✓ *Fathers Of Nations*
- ✓ *Silent Songs And Other Stories*
- ✓ *A Parliament Of Owls*
- ✓ *The Samaritan*

0746 222 000

OTHER SETBOOKS GUIDES AVAILABLE				
SETBOOK	**GUIDE**	**QUESTIONS & ANSWERS**	**VIDEOS**	**CONTACT**
Bembea Ya Maisha	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Mapambazuko Ya Machweo	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Nguu Za Jadi	✓	✓	✓	*0746-222-000*
	ENGLISH SETBOOKS			
Fathers Of Nations	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Silent Songs And Other Stories	✓	✓	✓	*0746-222-000*
A Parliament Of Owls	✓	✓	✓	*0746-222-000*
The Samaritan	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Artist Of The Floating World	✓	✓	✓	*0746-222-000*

0746 222 000

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

0746 222 000

CALL/TEXT/WHATSAPP

0746 222 000

OR

0742 999 000

0746 222 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

This is a Product of Mwalimu Consultancy Ltd.

0746 222 000

Powered by Mr Isaboke

0746 222 000

SUCCESS

0746 222 000

REGARDS

0746 222 000

0746 222 000